# NIFANYEJE ILI KUZUIA USAMBAAJI WA HOMA YA NGURUWE (AFRICAN SWINE FEVER)??






Upuliziaji wa dawa kwenye maeneo mbalimbali baada ya kutokea ugonjwa



**Ni muhimu kutambua yafuatayo kuhusu homa ya nguruwe**

- Huathiri wanyama jamii ya nguruwe
- unawapata nguruwe wa umri wote lakini nguruwe wadogo huathirika zaidi kuliko nguruwe wakubwa
- Unasambaa kwa haraka sana
- unasababisha vifo kwa wingi sana hasa pale unapotokea kwa mara ya kwanza katika eneo husika.
- Una sura tofauti ikiwa ni ya kuwa mkali kwa kipindi kifupi ama kuwa sugu.
- Ugonjwa hujitokeza kama mlipuko na katika maeneo ambayo uthibiti wake umeshindikana, hubaki katika eneo hilo kwa muda mrefu.
- Hakuna chanjo ya ugonjwa huu hivyo husababisha madhara makubwa kiuchumi kwa mmiliki wa nguruwe hivyo kuzuia ugonjwa huu ni muhimu sana.
- hauwapati binadamu.
- ni mgumu kutoka mara uingiapo katika eneo kama usambaaji wake hautathibitiwa kikamilifu na kuwa tishio kwa maeneo jirani.
- una mahusiano na kupe laini aina ya *Ornothodorus* ambao baada ya kung'ata mnyama mwenye virusi, hubaki na maambukizi kwa vizazi vyao vyote
- kupe wenye virusi huweza kuambukiza virusi kwa wanyama wa jamii ya nguruwe mwitu na wafugwao.
- sampuli zinatakiwa kuchukuliwa ili kuthitibisha aina husika

**Kisababishi cha ugonjwa.**

- maambukizi ya virusi viitwavyo African swine fever virus.
- dalili za ugonjwa hutofautiana kutokana ukali wa kirusi husika na pia jamii ya nguruwe aliyepata maambukizi.
- Katika, nguruwe wafugwao, virusi wakali husababisha ugonjwa unaouwa nguruwe wengi kwa siku chache baada ya kupata maambukizi.

**Tabia ya virusi visababishi**

- hufa katika joto la digree centigredi (°C) 56 kwa dakika 70 ama 60°C kwa dakika 30.
- hufa katika mazingira ya pH chini ya 3.9 ama zaidi ya 11.5 nje ya maji maji ya damu(serum).
- Serum inaongeza ustahimilivu wa virusi.

**Ustahimilivu wa virusi**

***Kemikali na dawa zinazopatikana ziuazo vijidudu (disinfectants)***: ulowekaji kwa dakika 30 ndani ya 8/1000 sodium hydroxide, hypochlorites – 2.3% chlorine,

3/1000 formalin, 3% ortho-phenylphenol huua vijidudu.
Pia madawa yenye ayodini.

Virusi hubaki ***hai nje*** ya mnyama ama kupe katika hali zifuatazo za hali joto ya kawaida (room temperature)
***Kinyesi*** kwa siku 11
***Mabanda yenye kinyesi*** - Siku 30
***Damu kwenye mbao*** - Siku 70
***Nyama iliyosindikwa kwa chumvi (cured hams)*** - Miezi 5 hadi 10
***Damu*** - Miezi 18

***Damu iliyooza na nyama iliyowekwa kwenye jokofu bila kugandishwa (chilled)*** - Siku 100
***Nyama iliyogandishwa katika ubaridi wa digrii sentigrade -20 ama chini zaidi*** - Miaka 15

**Hali ya ugonjwa ihusianayo na usambaaji wake**

Pindi mnyama apatapo maambukizi mara nyingi kupitia mfumo wa pua na mdomo, virusi huenea na kuzaliana kwa wingi ndani ya mwili wa mnyama kwenye chembe chembe hai zihusianazo zaidi na utengenezaji wa kinga za mwili katika matezi ya kichwa na shingo. Baada ya hapo, virusi husambaa mwili mzima kupitia damu na kuathiri mwili mzima vikiwemo matezi mengineyo na bandama.

Masaa 24 kabla ya dalili za ugonjwa kujitokeza na kipindi cha ugonjwa, virusi huwa vingi katika mwili na hutolewa mwilini kwa kupitia mfumo wa juu wa hewa, majimaji (secretions) (yakiwemo mate, malendalenda, machozi, mafua, ute) pamoja na uchafu mwingine utokao mwilini (excretions) kama mkojo, kinyesi na njia za uzazi.

**Katika hali ya ugojwa, vifuatavyo vinatunza virusi hai hivyo vyaweza kusambaza virusi**;

- damu, viungo na nyama, majimaji toka vungo va mwili wa nguruwe wagonjwa na waliokufa kwa ugonjwa;
- Wanyama waliopona baada ya kuugua homa ya nguruwe ama kupata maambukizi, hubaki na virusi hai katika kipindi kirefu cha maisha yao na kuwa chanzo cha virusi kwa wanyama wasiokuwa navyo. Hali hii inapatikana zaidi kwa nguruwe wafugwao katika maeneo ambayo ugonjwa umekuwa sugu bila kuisha na pia katika wanyama wa jamii ya nguruwe wasiofugwa hasa African wild swine;
- Kupe laini aina ya *Ornithodoros*.

**Homa ya nguruwe inavyoenea**

Ugonjwa unaenea kwa njia mbili; moja kwa moja ama kupitia vitu vingine.

***Kwa njia ya moja kwa moja***, virusi huenea kwa njia ya mgusano kati ya wanyama

wenye ugonjwa na wale wasionao, hasa kwa njia ya kupumuliana ama midomo.

***Kupitia njia zingine***, virusi husambaa na ugonjwa huweza kuaenezwa kwa njia zifuatazo:

i) Nguruwe kulishwa chakula/nyama iliyo na virusi hai

ii) Vitu vyenye virusi hai toka kwenye eneo lenye ugonjwa na kuingizwa kwenye banda lisililo na ugonjwa kupitia buti, viatu, nguo, vyakula, maji, majani ya kulalia n.k ambavyo katika njia moja ama nyingine vitaingia kwa myama aliyekuwa hana ugonjwa kupitia mdomoni, puani, hata kuchomwa

iii) Wanyama wazima kuwekwa kwenye maeneo yenye virusi hai ambamo nguruwe wenye virusi walikuwemo kama vile mabanda, magari n.k

iv) Nguruwe mwenye virusi anaweza kusambaza virusi vya ugonjwa huu akiumia na kutoka damu ambayo itaingia katika mnyama mwingine;

v) Damu, kinyesi, nyama iliyowekwa chiumvi na kukaushwa, nyama iliyogandishwa na nyama ya mifupa ni baadhi ya njia ambazo virusi vya ugonjwa huu husambaa endapo vitu hivyo vitakuwa vimeambukizwa

vi) Kuumwa na kupe aina ya Ornithodorus wenye virusi vya ugonjwa huu.

vii) Virusi waweza pia kusambazwa na wadudu wang'atao hadi masaa 24 tangu kula damu ya nguruwe mgonjwa

**Angalizo Muhimu**

Kwa kuwa virusi pia vinaweza kubebwa kwenye vifaa mbalimbali ikiwemo usafirishaji wa mazao ya nyama iliyo na virusi hai, binadamu na shughuli zake anaweza kuwa chachu ya kusambaa kwa ugonjwa huu. Nguo, viatu vyombo vilivyogusana na mate au udelele wa mnyama aliye na virusi vinaweza kusambaza virusi hivyo toka kundi/eneo moja hadi jingine. Nyasi zilizotunzwa kwa kulisha au kutandikia mifugo kama zitakuwa zimeguswa na mnyama mgonjwa zinaweza pia kuwa nyenzo ya kusambaza ugonjwa. Virusi vilivyo kwenye protini (ya damu, nyama, kinyesi, ndani ya mifupa) hubaki hai kwa muda mrefu. Aidha, . Hivyo viungo hivyo vinaweza kuwa chanzo cha kueneza ugonjwa huu kwa njia ya biaashara ya kimataifa.

Virusi pia vinaweza kuwepo hai katika mbegu za kiume 'semen' kwa muda wa siku 10, mate siku 11, Mkojo siku 7, maziwa siku 5, damu siku 5, Kinyesi siku 5 na mafua siku 7 kutoka nguruwe mgonjwa. Hivyo mazao haya kutoka mnyama mgonjwa yanaweza kusambaza ugonjwa huu.

Hizo ndizo sababu kubwa ya kuzuia biashara ya mifugo hai na mazao yake kutoka nchi zenye ugonjwa huu kwenda kwenye masoko ya nchi zilizoendelea.

**Tabia hatarishi ya ufugaji wa nguruwe inayoweza kuhatarisha wanyama kupata ugonjwa**

Ufugaji huru ama kuwafungia kwa kamba ama mabanda yasiyo na ubora






Epuka ufugaji hatarishi na kujenga mabanda bora ya nguruwe yenye udhibiti na watu kutoweza kuingia kwa urahisi.

| | |
|---|---|
|  | Machinjio ya nguruwe ni moja ya maeneo hatarishi kwa kuwa damu ya mnyama mwenye maambikizi ni chanzo kikuu cha virusi na huweza kuwafikia nguruwe kupitia mavazi, vifaa vya uchinjaji n.k hivyo ni muhimu machinjio yafungwe pindi utokeapo ugonjwa ili kuzuia usambaaji wake. |

**Njia za kuzuia na kudhibiti homa ya nguruwe pindi utokeapo mlipuko eneo jirani ili kuepuka uwezekano wa maambukizi kuenea**


Sheria za kusafirisha wanyama kutoka eneo moja na jingine ifuatwe kwa makini na kanuni za ufugaji bora wa nguruwe zitolewe kwa wafugaji toka kwa afisa mifugo aliyeko katika eneo.

- Vipeperushi, vijarida na mabango yanayoelezea ugonjwa, athari za ugonjwa na tahadhari za kuchukua visambazwe
- Nguruwe wafugwe ndani ya mabanda bora na wasiachiwe wazurure **marufuku ufugaji wa nguruwe huria au kufunga kamba**
- Usinunue nguruwe, nyama na vyakula kutoka maeneo yenye ugonjwa
- Chakula wanachopewa nguruwe kipikwe kuzuia virusi kusambaa kwa mfano, nyama isiyosindikwa iwekwe jikoni kwa muda wa dakika 30 katika joto la nyuzi joto 70°C.
- Zuia wageni kuingia katika mabanda ya nguruwe
- Usiingize nguruwe wapya au kuwatoa kwenye mabanda
- kupiga marufuku mara moja uchinjaji wa nguruwe katika eneo
- kupiga marufuku uingizaji na utoaji wa nguruwe na mazao yake katika eneo

**Hatua zingine za tahadhari dhidi ya ugonjwa wa homa ya nguruwe pindi ugonjwa utakapotokea**

- Tenganisha nguruwe wagonjwa na wazima
- Chinja na kufukia vizuri mizoga ya nguruwe walioathiriwa.
- Mabanda yote yaliyokuwa na nguruwe waliokufa kwa ugonjwa yapuliziwe dawa aina ya virkon au formaldehyde au sodium hypochlorite au nyingine inayofaa
- Mabanda yaliyotumika kutunza wanyama wagonjwa yasiingizwe nguruwe wapya hadi karantini itakapoondolewa na ruhusa ya kufuga tena kutolewa na daktari wa mifugo
- Uingizaji wa vyakula vya mifugo vyote upate kibali cha Daktari wa Mifugo aliyeidhinishwa

- Kuona uwezekano wa kuangamiza nguruwe wote katika eneo lililoathirika ili kudhibiti ugonjwa usienee katika sehemu nyingine





Jenga na kufuga nguruwe kwenye mabanda bora yenye udhibiti dhidi ya kuingiliwa kirahisi.

**Baadhi ya hatua za kuchukuliwa na uongozi wa wilaya/manisipaa/halmashauri**

(i) Kufuatilia utekelezaji wa kanuni bora za ufugaji wa nguruwe.

(ii) Kuteua vituo vya ukaguzi (Check points) katika wilaya na kuhakikisha ukaguzi unafanyika kwa makini.

(iii) Daktari wa Mifugo wa Wilaya atateua watumishi ambao watafanya ukaguzi wa mifugo na vyakula vya mifugo katika vituo vituo vya ukaguzi vilivyowekwa muda wote.

(iv) Kuandaa mabango ya kuelimisha na kuhamasisha juu ya ugonjwa na kuyaweka katika sehemu ambazo zilianishwa zitaleta tija

(v) Kutoa elimu juu ya ugonjwa kwa matangazo mbalimbali ili wafugaji wawe na uelewa wa namna ya kudhibiti ugonjwa wa Homa ya Nguruwe.

(vi) Kuandaa orodha ya wafugaji na idadi ya nguruwe wanaofugwa katika kaya na kufuatilia ufugaji huo.

(vii) Kuwaorodhesha waingizaji, wasambazaji, na wauzaji wa vyakula vya mifugo katika wilaya na kutoa elimu juu ya udhibiti wa ugonjwa wa Homa ya Nguruwe.

## Kijarida hichi kimetayarishwa na watumishi toka:


Wakala wa Maabara za Mifugo Tanzania (TVLA)
S. L. P. 9254, DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu: +255 22 – 2863104, +255 22 2861152
Nukushi: +255 22 2864369
Barua pepe: ce-tvla@tvla-tz.org; info@tvla-tz.org

Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)
Kitivo cha Tiba ya Mifugo
S.L.P 3015, Chuo Kikuu, Morogoro, Tanzania.
Simu: +255 23 260 4647/260 3511- 4
Nukushi: +255 23 260 4647

Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi



**Chini ya mradi uliofadhiliwa na:**

**Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia**

**Kupitia**

**Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania**

**Picha zimetolewa kwa hisani ya Dr. Gerald Misinzo na Tebogo Kgotlele wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Dr. Emmanuel Macha wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Dr. C.A.R. Ngeleja wa TVLA**